- Utafiti ufaao wa Ufunuo si zoezi la fumbo(usiri) au dhana zisizo na msingi
  - Ni zoezi la uchunguzi makini wa maandishi pamoja na utafiti wa hatua kwa hatua wa Maandiko.
    - Wiki iliyopita katika Sura ya 1 tuliona jinsi somo letu linavyoweza kuwa la hatua kwa hatua wakati tuliona yale ambayo Yohana aliandika
    - Kwanza, tuliona kwamba Yohana aliambiwa aandike anayoyaona, si yale anayoambiwa
  - Na maelezo hayo yalieleza kwa nini kitabu hiki ni kigumu kukielewa
    - Kwa kawaida, kutafsiri Biblia humaanisha kutafsiri maelezo
    - Lakini katika kisa hiki, Yohana hutoa tu maelezo ya matukio ambayo anaona
    - Ambayo ina maana ni lazima kwanza tuelewe kile anachoeleza, na kisha tunapaswa kutafsiri maana ya maono yake
  - Mtindo huu wa kusoma Maandiko unathamini sana ustadi wetu wa uchunguzi na maarifa (ujuzi) yetu ya Maandiko kwa ujumla.
    - Ustadi wetu wa uchunguzi utatusaidia kupata maana ya matukio ambayo Yohana anatuelezea
    - Na ujuzi wetu wa Biblia unakuja katika kufasiri maono
  - Na hilo ndilo jambo la pili tulilojifunza juma lililopita...maana ya alama zilizotumika katika kitabu hiki zitapatikana mahali fulani katika Maandiko.
    - Ikiwa maana ya ishara ni muhimu kwa hadithi, basi Biblia itakuwa imeieleza mahali fulani kwa manufaa yetu
    - Na mara nyingi maelezo hayo yatapatikana katika muktadha wa karibu
- Na kisha, cha tatu na hatimaye, tulijifunza kwamba kitabu chenyewe kina muundo rahisi sana lakini muhimu ambao utaongoza uelewa wetu
  - Muundo huo umetolewa katika muhtasari ambao Yesu alimpa Yohana katika Sura ya 1
    - Muhtasari unapatikana katika mst.19, na tuliuchambua wiki iliyopita
    - Lakini tulikuwa na kazi ambayo haijakamilika ndani yake, kwa hiyo hebu turudi na kuanza somo letu usiku wa leo huko

> UFU. 1:19 Basi, uyaandike mambo hayo uliyoyaona, nayo yaliyopo, na yale yatakayokuwa baada ya hayo.

- Yohana aliambiwa na Yesu kuandika kitabu hiki katika sehemu tatu
  - Sehemu ya kwanza ilikuwa: Andika mambo uliyoyaona
  - Sehemu ya pili ni: andika mambo yaliyopo
  - Na sehemu ya tatu ndiyo hii: Andika mambo yatakayotokea baada ya hayo
- Wiki iliyopita tulitambua sura za kitabu zinazolingana na kila sehemu hizi
  - Na tulifanya hivyo kupitia uchunguzi rahisi tukianza na wakati wa vitenzi alivyotumia Yesu
    - Sehemu ya kwanza Yesu aliita kitu ambacho Yohana alikuwa amekiona
    - Yesu alitumia kitenzi cha wakati uliopita, kwa hiyo Yesu alikuwa anarejelea mambo ambayo

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

Yohana alikuwa ameyaona tayari tunapofikia mst.19

- Yohana alikuwa ameona nini kufikia wakati wa Sura ya 1:19 ?
    - Jibu la wazi ni mambo yaliyotukia kabla ya mstari huo, ni mambo ambayo Yohana alieleza katika Sura ya 1
    - Kwa maneno mengine, Sura ya 1 ni sehemu ya kwanza ya kitabu, mambo ambayo Yohana alikuwa ameona
- Na Yohana aliona nini? Alimwona Yesu katika umbo Lake la ufufuo na utukufu
    - Naye akaona vinara vya taa na nyota mkononi mwa Yesu
    - Alieleza yote aliyoyaona na jinsi maono hayo yalivyomjia
- Na katika maelezo haya yote, Yohana anatoa mamlaka kwa kile anachoandika, ambayo ndiyo ilikuwa hoja katika Sehemu ya 1
    - Kuanzia na mlolongo wa ulinzi na utambulisho wa Yohana kama mtume na kisha kuelekea jinsi Yohana alivyokutana na Kristo.
    - Hatimaye tukihitimisha kwa kuonekana kwa Yesu na maelekezo yake kwa Yohana...kwa maelezo haya yote tuna ujasiri wa kuukubali ushuhuda wa Yohana.
    - Ikiwa tunakubali uhalali wa Maandiko hata kidogo, basi tuna sababu sawa ya kukubali ukweli wa maelezo ya Yohana

- Sasa tunahamia kwenye mambo yaliyopo, na kama Sehemu ya 1 ni rahisi kutambua ni sura zipi zinazohusishwa na Sehemu ya 2.
    - Sehemu ya pili lazima ianze katika Sura ya 2, kwa kuwa Sehemu ya 1 ilijumuisha tu mambo ambayo Yohana alikuwa ameona kabla ya mst.19
        - Kwa hivyo Sehemu ya 2 inaishia wapi na Sehemu ya 3 inaanzia wapi katika maandishi ya Ufunuo?
        - Jibu rahisi ni kwamba ikiwa tungeweza kutambua sehemu ya 3 ilianza wapi, basi kwa mchakato wa kuondoa tungejua hivyo vyote.
        - Kwa ufafanuzi Sehemu ya 2 inaishia pale ambapo Sehemu ya 3 inaanza
    - Kama tulivyoona wiki iliyopita, kuna kidokezo dhahiri katika kifungu kinachotuambia sehemu ya 3 inaanzia wapi:

> UFUNUO 4:1 Baada ya hayo naliona, na tazama...

- Yesu aliita Sehemu ya 3 “mambo yatakayotukia baada ya hayo”
- Na kisha tunapata maneno hayo muhimu kuanza Sura ya 4, ambayo si bahati mbaya….ni alama tunayopaswa kutambua.
- Yanatuambia kuwa Sura ya 2 & 3 ni Sehemu ya 2; mambo "yaliyopo"
- Lakini neno "yaliyopo" linaleta mkanganyiko fulani kwetu katika hatua hii
    - Kitenzi hicho cha wakati wa sasa kinaonekana kudokeza kwamba Yesu alikuwa akimwonyesha Yohana mambo ambayo yalikuwa muhimu tu katika siku za Yohana
    - Lakini hiyo si kweli...kulingana na muhtasari ambao Yesu alitupa, mambo ya Sehemu ya 2 lazima

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

yaendelee kuwa muhimu hadi Sehemu ya 3 ianze.

- Kimantiki, mambo “yaliyopo” (Sehemu ya 2) yataendelea kuwa kweli (yaani, kubaki “yapo”) hadi mambo yatakayotokea (Sehemu ya 3) yaanze.
  - Zaidi ya hayo, tunapotazama yale ambayo Sura ya 2 & 3 inayo, ni jambo linaloleta mantiki kwa nini Yesu aliita sehemu hii ni mambo "yaliyopo"
  - Kwa sababu katika sura hizi tuna barua zilizoandikwa kwa kanisa, ambazo ni kwako na mimi
- Kwa hiyo ushauri wa Yesu uliotolewa kwa kanisa lake lazima ubaki kuwa kweli na kuwa na matokeo maadamu kanisa lake lenyewe bado lipo.
  - Kwa hiyo katika siku za Yohana, barua ambazo Yesu aliandika kwa Kanisa ni mambo ambayo “yapo” kwa ajili ya kanisa
  - Vivyo hivyo, barua ambazo Yesu aliandika kwa Kanisa ni mambo ambayo "yapo" kwa kanisa leo
  - Ni baada tu ya matukio yanayotajwa katika Sura ya 4 na kuendelea ndipo tunaweza kusema kwamba mambo “yaliyopo” yamekwisha
- Kwa hiyo hebu tuingie katika Sehemu ya 2 na kuelewa ushauri wa Yesu kwa Kanisa lake, mambo yaliyopo, barua saba zilizoandikwa kwa makanisa saba ya siku za Yohana.
  - Kuanza kwa kufahamu (kuelewa) jinsi tunavyopaswa kukaribia tafsiri ya barua hizi
    - Kulingana na muundo wa barua hizi na yaliyomo ndani yake, tunapaswa kutumia njia tatu zinazojenga tafsiri kwa ushirikiano.
    - Njia zote tatu ni halali na kila moja hutupatia utambuzi wa kipekee ambao Yesu alitaka tuwe nao
  - Kwanza, lazima tusome barua hizi kihalisi, tukizichukukulia kwa maneno yake halisi (yaani kile kinachosemwa moja kwa moja).
    - Ni barua halisi, zilizoandikwa na Yesu kupitia mkono wa Yohana
    - Zilikuwa na wasikilizaji halisi akilini, wanaume na wanawake walioishi katika siku za Yohana
    - Barua hizi zilifika kwa wale waliokusudiwa huko Efeso, Smirna, na mahali pengine kama vile Yesu alivyokusudia.
  - Na mambo ambayo Yesu alizungumza kwa kila moja ya makanisa haya yalikuwa ya kweli kwa kila jumuiya
    - Efeso ilikuwa imesimama imara dhidi ya walimu wa uongo
    - Smirna ilikuwa ikiteswa, na kadhalika
    - Kwa maana hiyo, barua hizo ni mahususi na za kihistoria
  - Lakini kama tulivyojifunza, barua sio tu za kihistoria katika mwelekeo
    - Barua zinaendelea kuwa na umuhimu wa siku hizi (“zipo”) kwa Kanisa, hata miaka 2,000 baadaye.
    - Zaidi ya hayo, tunakumbuka kwamba Yesu alitupa barua saba haswa, na namba saba katika Biblia inawakilisha 100%.
    - Kwa hiyo barua hizi ziliandikwa kwa kanisa zima, sio tu jumuiya saba za nyakati za kale
  - Kwa hiyo lazima pia tuelewe kwamba barua hizi pia zinazungumza na hali na mitazamo ambayo inabaki kuwa kweli wakati wote wa kanisa.

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

        - Katika kila wakati, mahali fulani ulimwenguni tunaweza kupata jumuiya ya kanisa inayopitia masuala sawa na Efeso au Smirna.
        - Siku zote kuna makanisa yanayopigana na walimu wa uongo, mateso, ukengeufu n.k.
        - Na barua hizi huleta faraja, hekima na marekebisho kwa hali hiyo kama zilivyofanya katika siku ya Yohana
        - Kwa hiyo, barua hizo ni za ulimwengu wote na hazina wakati katika matumizi
- Lakini bado kuna njia moja zaidi ambayo lazima tuelewe barua hizi, na njia hii ya tatu ni rahisi kupuuza
    - Tunajua kitabu cha Ufunuo ni unabii, lakini unabii haukomei kwenye Sura ya 4 na zaidi.
        - Kila sura katika kitabu ina kipengele cha kinabii
        - Kwa mfano, ingawa Sura ya 1 ilirekodi tukio lililopita, hata hivyo ilijumuisha maelezo ya kinabii
        - Kuonekana kwa Yesu katika umbo la utukufu ni kinabii katika kutuonyesha kuonekana kwa Yesu wakati ujao atakaporudi
        - Kwa hakika, hilo ndilo kusudi la kitabu kizima: kutuonyesha matukio yatakayofuatana na ujio wa pili wa Yesu.
        - Na kila sura inachangia kusudi hilo kwa namna fulani
    - Kwa hiyo ni lazima tutafute vipengele vya kinabii katika barua zilizotolewa kwa makanisa na kwa uchunguzi wa makini tunazipata
        - Inahitaji turudi nyuma na kupata muhtasari wa  zote
        - Ili kufanya hivyo, ninatumia mchoro rahisi kuwakilisha Sehemu ya 2 ya Ufunuo, mambo ambayo yapo katika Sura ya 2 & 3.
    - Hebu tuanze kwa kuangalia maeneo ya makanisa haya saba katika siku za Yohana
        - Yote yalikuwepo Asia Ndogo, Uturuki ya sasa ya Kusini-Magharibi
        - Kuyatazama kwenye ramani kunaonyesha mtindo unaovutia
        - Mpangilio wa barua hizo unaendana na mzunguko wa saa
        - Mtindo huo unaonyesha kwamba barua hizo ni kiwakilishi cha kupita kwa wakati
    - Sasa mwanafunzi mwerevu wa historia anaweza kusema kwamba saa za mitambo zilikuwa hazijavumbuliwa hadi karne ya 14.
        - Lakini vipimo vya jua (miale ya jua) vimekuwa vikitumika tangu 3,500 KK
        - Na watazamaji wa jua hufuatilia mwendo wa jua kwenye uso wa saa
        - Wakati ikitazamwa kutoka ncha ya Kaskazini, dunia inazunguka kwa mwelekeo wa  kinyume cha saa
        - Hivyo basi vipimo vya jua (miiale ya jua) vinaonyesha mzunguko wa jua kwa mwelekeo/mwendo wa saa, jambo ambalo Warumi walilielewa kuhusu mwendo wa wakati
        - Baadaye, watengenezaji wa saa wa kwanza waliamua kuonyesha kupita kwa wakati kwa mwelekeo ule ule ili kuendana na vipimo vya jua (miale ya jua) vya siku hizo.
- Kwa hiyo jiografia ya kupendeza ya barua hizi inapendekeza kuwa zinawakilisha jinsi kanisa

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

linavyobadilika kulingana na wakati wa nyakati (enzi) ambazo "zipo"

- Kwa maneno mengine, barua zina mtazamo wa kinabii ambao ni ishara unahusiana na mwisho wa nyakati (eskatolojia).
    - Eskatolojia inahusu mafundisho ya siku za mwisho
    - Na barua hizi zinatuelekeza kwenye wakati huo
    - Jinsi gani? Wanaunganisha nukta kati ya matukio ya siku ya Yohana na matukio ya kurudi kwa Kristo
    - Zinatuambia jinsi Kristo anavyouhamisha ulimwengu kutoka ujio wake mara ya kwanza hadi Ujio Wake mara ya Pili
- Na ndio maana Yesu alikiita kipindi hiki kuwa ni nyakati “zilizopo” kwa sababu zinabaki kuwa siku hadi tufikie matukio ya mwisho.
    - Kanisa la karne ya kwanza lilikuwa katika hali ile ile tuliyo nayo sasa
    - Kama vile walivyokuwa wakingojea kurudi kwa Kristo ndivyo tulivyo leo
    - Sura ya 4-22 zinaeleza jinsi matukio ya mwisho ya wakati huu yataenda, jinsi Yesu atakavyorudi na kile kinachokuja baada ya hapo
    - Wakati Sura ya 2 na 3 zinaeleza matukio ambayo lazima yatendeke kati ya karne ya kwanza na nyakati za mwisho
- Lakini kwa jinsi ambavyo Yesu ameunda unabii huu, haikuwa dhahiri kwa Kanisa mara moja kwamba tunapaswa kuona barua katika maana hii ya tatu.
    - Ubora wa eskatolojia wa barua ulibaki kufichwa kwa kanisa kwa zaidi ya miaka 2,000 iliyopita.
    - Ni katika kipindi cha miaka 150 tu au zaidi ambapo tafsiri ya kinabii imeshika hatamu kanisani
    - Na nikuonyeshe kwa nini Kristo alikusudia iwe hivyo

- Tutakapochunguza kila moja ya barua, tutaona kwamba barua hufuata muundo maalum
    - Kila barua itakuwa na vipengee fulani, na vipengele hivi vinawiana katika zote saba
        - Kutokana na muundo huo, tutaanza kuona jinsi kila barua inawakilisha kipindi cha historia ya kanisa
        - Kwa maneno mengine, kipindi chote cha wakati wa kanisa linapokaa duniani kinawakilishwa na barua hizi saba
        - Sio tu kwamba namba "7" inaashiria 100% ya kanisa, pia inawakilisha 100% ya wakati wa kanisa duniani.
    - Tunaweza kuwakilisha sehemu saba za wakati wa kanisa kwa mchoro rahisi
        - Kila moja ya barua inawakilisha urefu fulani wa muda wakati wa enzi ya kanisa duniani
        - Na kwa pamoja, barua zote saba zinaeleza jumla ya muda (100%) wa kuwepo kwa kanisa duniani kabla ya kurudi kwa Yesu.
    - Tukizitazama barua hizi mapema, haingewezakana kabisa kujua ni muda gani kila mojawapo ya vipindi saba ingetawala
        - Kwa kweli, hatungeweza hata kujua kama barua hizi zinawakilisha vipindi vya historia hata

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

kidogo

        - Lakini tukitazama nyuma, tunaweza kuona jinsi yaliyomo katika barua hizo yanavyopatana na matukio katika historia
        - Na kwa kulinganisha maelezo ya kila herufi na matukio katika historia, tunaweza kupata mapumziko kati ya kila herufi
        - Tunaweza kutambua matukio yanayomaliza  kipindi kimoja kati ya vile saba na kuanzisha kingine.
- Kwa hiyo njia ya tatu ya kufasiri barua ni ya kinabii, tukitambua kwamba barua hizo zinasimama kwa kipindi fulani cha historia.
    - Na mtazamo huu unatuongoza kwenye hitimisho tatu za kuvutia
        - Kwanza, inaeleza kwa nini tafsiri ya kinabii ililikwepa kanisa kwa zaidi ya miaka 2,000 iliyopita
        - Kwa sababu ilihitaji kutazama mambo yaliyopita ili kuithamini
        - Ni kufikia karne ya kumi na tisa tu ambapo wasomi walianza kuona muundo na kuona uhusiano na wakati wa kanisa
    - Pili, mtazamo huu unapendekeza kwamba kama vile Kanisa lilivyokuwa na mwanzo (wakati wa Pentekoste) hivyo litakuwa na hitimisho kwa namna fulani.
        - Kama Efeso ilianzisha wakati wa kanisa basi Laodikia ndiyo inaumaliza
        - Hilo linatupeleka kwenye maswali kama jinsi gani na kwa nini kanisa linafika mwisho na hilo linamaanisha nini kwetu?
        - Na nini kinafuata? Kitabu cha Ufunuo kinajibu maswali hayo
    - Hatimaye, mara tunapotambua kwamba enzi ya kanisa ina hatua saba tu, inakuwa inawezekana kuelewa jinsi tulivyo karibu na mwisho
        - Ikiwa ungeniambia tunaishi katika hatua ya 3 au hatua ya 4, ningejua tuna muda mwingi uliobaki hadi mwisho wa umri.
        - Hata hivyo wazo hilo linaenda kinyume na Maandiko, sivyo?
        - Tunaweza kufikiria mistari ambayo inatukumbusha kuwa daima tuwe tayari kwa ajili ya kurudi kwa Kristo kwa sababu ni tukio ambalo linaweza kutokea wakati wowote.
    - Na ndio maana mbinu hii ya kutafsiri barua kwa makanisa haikufunuliwa kwa kanisa hadi karne ya kumi na tisa.
        - Kwa sababu sisi ni kipindi cha wakati wa kanisa kinachohitaji kujua kuhusu muundo huu
        - Na tunapoanza kusoma barua utaona ni kwa nini
- Kwa hivyo, hebu tusogee sasa kwenye barua zenyewe, na ya kwanza tunayojifunza itaweka kielelezo kwa zingine zote

---

UFUNUO 2:1 Kwa malaika wa kanisa lililoko Efeso andika; Haya ndiyo anenayo yeye azishikaye hizo nyota saba katika mkono wake wa kuume, yeye aendaye katikati ya vile vinara saba vya dhahabu.
UFU. 2:2 Nayajua matendo yako, na taabu yako, na subira yako, na ya kuwa huwezi kuchukuliana na watu wabaya, tena umewajaribu wale

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

wajiitao mitume, nao sio, ukawaona kuwa waongo;
UFUNUO 2:3 tena ulikuwa na subira na kuvumilia kwa ajili ya jina langu, wala hukuchoka.
UFUNUO 2:4 Lakini nina neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza.
UFU. 2:5 Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu.
UFUNUO 2:6 Lakini unalo neno hili, kwamba wayachukia matendo ya Wanikolai, ambayo na mimi nayachukia.
UFUNUO 2:7 Yeye aliye na sikio, na alisikie neno hili ambalo Roho ayaambia makanisa. Yeye ashindaye, nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katika bustani ya Mungu.

- Barua hizi saba zina muundo wa hali ya juu, na muundo huo hurudia kutoka barua moja hadi barua nyingine, na hurahisisha kujifunza.
  - Makanisa yana majina ya miji, na barua huanza na salamu
  - Kisha Yesu anatoa sifa, lawama, mawaidha, ahadi na maonyo
- Kwa hiyo tutachambua kila barua kulingana na muundo huu na tutachunguza kila barua kutoka kwa mitazamo yote mitatu
  - Tutaangalia kila moja kutoka kwa mtazamo halisi, wa kihistoria
  - Mtazamo wa ulimwengu wote, wa milele
  - Na hatimaye, kwa mtazamo wa kinabii, kieskatolojia
- Na tunaanza na jina la kila kanisa na mpangilio wake wa kihistoria
  - Efeso lilikuwa jiji la bandari lililokuwa kwenye Bahari ya Mediterania
  - Jina lake lilimaanisha "kuhitajika" au "kutamanika"
  - Ilikuwa mojawapo ya bandari kuu zinazounganisha ncha za Mashariki na Magharibi za Milki ya Roma
  - Mtiririko mkubwa wa bidhaa kupitia bandari hii ulisaidia kufanya jiji kuwa tajiri sana
- Bandari za baharini huleta meli na meli huleta mabaharia na wasafiri, kwa hiyo jiji hili lilikuwa na mahekalu mengi yaliyowekwa kwa miungu mingi ya Waroma.
  - Kubwa zaidi lilikuwa hekalu la Artemi au Diana lililojaa makahaba
  - Na katikati ya jiji hili lenye shughuli nyingi, tunalo pia mojawapo ya makanisa makubwa zaidi yenye ushawishi mkubwa katika karne ya kwanza.
  - Iliwahesabu Paulo, Yohana na Timotheo miongoni mwa viongozi wake kwa miaka mingi na inaangaziwa sana katika kitabu cha Matendo ya Mitume na katika Nyaraka.
- Yesu analihutubia kanisa kwa kujiita yeye "Mwenye nyota saba katika mkono Wake wa kulia", akitembea kati ya vile vinara saba vya taa vya dhahabu.
  - Hapa tunaona muundo mwingine muhimu katika barua, ambapo Yesu anaweka kipengele kutoka

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

kwa maelezo ya Yohana katika Sura ya 1 kwa kila kanisa.

    - Kipengele maalum ambacho Yesu anachagua kwa kila kanisa kinatuambia jambo fulani kuhusu hali ya kanisa hilo
    - Katika kisa hiki, Yesu anaweka alama za nyota na vinara vya taa
  - Kutokana na somo letu kwa juma lililopita, tulijifunza kwamba taswira ya nyota inawakilisha malaika chini ya mamlaka ya Kristo wakiwahudumia watakatifu.
    - Na vinara vya taa vinawakilisha jukumu la kanisa kuwakilisha ukweli wa Kristo kwa ulimwengu, kuleta nuru gizani
    - Picha ya Kristo akiwa amesimama katikati ya taa na kushikilia nyota inaonyesha mamlaka yake ya kutawala juu ya Kanisa.
  - Hivyo ukumbusho usio na kificho kwa Efeso unaonekana wazi kuwa huu: Yesu ndiye aliye madarakani, na bado anaongoza mwelekeo wa kila kitu.
    - Kanisa ni lake na analiamuru hata kutoka Mbinguni
    - Anataka kanisa la Efeso kukumbuka hilo, na inakuwa wazi tunapotazama kile Yesu analiambia kanisa.
  - Yesu anaanza kwa kuupongeza mwili huu, akisema wanataabika kwa kustahimili wakifanya matendo ya namna moja au nyingine.
    - Zaidi ya hayo, hawawezi kuvumilia watu waovu wanaokuja wakijiita mitume lakini sio
    - Wanawajaribu watu kama hao na kuwagundua kuwa waongo, kwa hiyo Yesu anawapongeza kwa kujitolea kwao kwa mamlaka ya kweli
    - Hatimaye, wanavumilia na kustahimili kwa ajili ya jina la Kristo bila kuchoka
- Kanisa hili kwa hakika linaonekana kuwa mfano mzuri, na tunaweza kulitumia kama funzo linaloweza kutumika kwa kila kanisa.
  - Kila kanisa linapaswa kuwajaribu wale wanaokuja kwa mamlaka au mafundisho
    - Katika kesi ya mtu anayejiita mtume, mtihani ulikuwa ikiwa ana nguvu za mitume
    - Mitume walikuwa wanaume walioagizwa baada ya Yesu kuwatokea binafsi, kwa kuwa Yesu mwenyewe ndiye ambaye huwateua mitume kwa njia ya kujionyesha binafsi.
  - Katika karne ya kwanza, mtume alikuwa na nguvu na mamlaka ya pekee
    - Mitume walikuwa na nguvu za miujiza na kuandika Maandiko kulingana na uongozi wa Roho
    - Kristo aliwateua wale kumi na wawili wa kwanza alipokuwa hai, na aliwateua wengine zaidi baada ya kufufuka
    - Lakini Yesu aliacha kuwaweka rasmi Mitume wakati fulani katika karne ya kwanza, na mtume wa mwisho kufa alikuwa Yohana
  - Na wakati huo, watu wa uongo walijaribu kujiita mitume kwa matumaini ya kupata vyeo vya mamlaka juu ya kanisa
    - Lakini makanisa kama Efeso yalikuwa makini na yakiangalia kwa uangalifu mafundisho, na yalijua vyema kuliko kuamini madai kama hayo
    - Ikiwa mtu hangeweza kutoa ishara za miujiza zinazofanana na mitume wote, basi kanisa lilijua kwamba watu hawa hawakuwa wa kweli.

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

        - Waliwajaribu, na wanaume hao waliposhindwa kufaulu mtihani huo, wakatolewa nje ya kanisa
    - Ingawa mitume hawatembei tena duniani, bado tunahitaji kufuata mfano wa Efeso katika kuwajaribu wale wanaojitolea kutufundisha au kutuongoza.
        - Hakuna aliye mkamilifu, lakini tunatafuta matunda mazuri katika maisha yao na tunajaribu mafundisho yao kwa Biblia
        - Na tunapofanya hivyo, tunampendeza Kristo, kama vile alivyowasifu wale wa Efeso
- Angalia katika mst.6 Yesu anasema wanachukia matendo ya Wanikolai
    - Wanazuoni wanajadili maana ya kauli hii
        - Tunajua jina hilo linamaanisha "mshindi juu ya watu", maana ambayo inapendekeza harakati ya kushinda mkutano
        - Kwa hiyo wengi wanaamini kwamba Wanikolai walikuwa wakianzisha uzushi wa tabaka tawala katika kanisa linaloitwa makasisi.
    - Lakini Biblia haipendekezi kamwe wala kuunga mkono utengano huo
        - Hakuna kitu kama makasisi dhidi ya walei
        - Mwili wa Kristo ni mmoja, na sisi sote ni makuhani Biblia inasema
    - Ndiyo tunao viongozi kanisani, lakini hawana utakatifu wake kipekee wala hawalindi njia ya kumfikia Mungu kwa niaba yetu
        - Wao wanalitumikia kanisa kwa karama walizopewa, kama amabvyo sisi pia tunalitumikia kanisa kwa karama tulizopewa.
        - Wana mamlaka na tunaheshimu mamlaka hayo, lakini kama watu binafsi hawajatengwa na sisi wengine
    - Hatimaye, tunaweza kujifunza somo kutokana na uvumilivu na ustahimilivu wa Efeso katika kazi ya kumtumikia Kristo
        - Yesu anabainisha kuwa wana matendo, na wanatimiza matendo haya mfululizo na bila kuchoka
        - Hiyo ni pongezi kubwa, kwa sababu hilo ni jambo gumu kufanya
        - Wengi wetu tuna hamu ya kuingia haraka katika kumtumikia Yesu, lakini jaribio la kweli la utumishi lipo katika kuendelea kushikamana na kazi hiyo
    - Biblia inasema uvumilivu ni kiungo kikuu cha ukomavu wa kiroho na thawabu ya milele

> YAKOBO 5:11 Angalieni, twawaita heri wao waliosubiri. Mmesikia habari ya subira yake Ayubu, mmeuona mwisho wa Bwana ya kwamba Bwana ni mwingi wa rehema, mwenye huruma.

> EBR. 10:35 Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana una thawabu kuu.
> EBR. 10:36 Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kuyafanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi.

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

- Kwa hiyo Efeso ni mfano kwetu wa utambuzi, umoja na uvumilivu
    - Lakini si kila kitu kilikuwa kamili katika kanisa hilo, kwa kuwa Yesu pia alikuwa na baadhi ya hoja za kuwakosoa.
        - Na katika mojawapo ya kauli za kustaajabisha na zenye kustaajabisha katika Biblia yote, Yesu anasema kanisa hili lilikuwa limeacha upendo wake wa kwanza
        - Taarifa hiyo inavutia sana na mwanzoni inaonekana rahisi kuelewa
    - Kwa wazi, "upendo wa kwanza" wa kanisa lazima urejelee kwa Yesu, kwani ni upendo gani mwingine huja kabla ya upendo wa mwamini kwa Yesu?
        - Hata hivyo, tunashangaa ni jinsi gani hili liinaweza kuwa kweli kwa kanisa lililovumilia kwa ajili ya jina la Kristo?
        - Walipinga walimu wa uongo waliojaribu kuwagawanya, na bado walisahau kanisa lilikuwa nini?
        - Jinsi gani hasa walipoteza upendo wao wa kwanza?
    - Barua hiyo inatupa vidokezo kadhaa vya kutusaidia kuelewa hali hiyo, tukianzia na maelezo ya Yesu
        - Yesu analikumbusha kanisa kuwa yeye ndiye anayetawala kanisa lake
        - Naye hutumikia kanisa lake kwa njia ya malaika chini ya mamlaka yake
    - Kwa hiyo tunapata mkanganyiko huu wa kuvutia: kanisa lilikuwa kinzani sana kwa viongozi wa uongo na wale waliotaka kuanzisha tabaka maalum la watawala.
        - Hata hivyo Kristo aliona hitaji la kuwakumbusha kuwa alikuwa anaongoza
        - Inaonekana kwamba upinzani wao dhidi ya kuongozwa na viongozi wa uongo ulikuwa umebadilika na kuwa kutotaka kutawaliwa na Kristo pia.
    - Walibaki bila upendo wao wa kwanza kwa namna ambayo kijana hubadilika kutoka utii hadi ukaidi
        - Wanabadilika kutoka kutegemea na kuthamini uangalizi na msaada wa mzazi hadi kukasirika chini ya mamlaka ya mzazi huyo.
        - Wameacha mapenzi yao ya kwanza kwa maana ya kwamba walisahau siku za mwanzo za uhusiano huo na wamechukulia kawaida.
- Dokezo la pili la kuunga mkono hitimisho hili linapatikana katika tiba ambayo Yesu analipatia kanisa katika mst.5
    - Yesu anawaambia wakumbuke pale walipoanguka, na kufanya matendo waliyofanya hapo kwanza
        - Wanapaswa kufikiria juu ya makosa yao na kutubu makosa yale ya zamani
        - Wito wa kutubu unamaanisha kutafakari upya njia yao ya sasa, kuunga mkono na kusonga kwa njia bora zaidi
    - Dawa ya Yesu ni ya kuvutia hasa tunapokumbuka aliwapongeza tu kwa matendo yao ili tujue walikuwa hai
        - Na bado, shughuli hiyo haikuwa shughuli sahihi, haikuchochewa na upendo wao kwa Kristo
        - Kwa maneno mengine, mahali fulani njiani, jumuiya hii ya kanisa ilipoteza kuona kwa nini

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

Kristo aliweka kanisa lake duniani

- Waliacha upendo wao wa kwanza, na kanisa likawa juu ya kitu kingine isipokuwa Yesu na Injili yake
- Walikuwa na shughuli nyingi sana na walivumilia katika kazi hiyo kwa ajili ya jina la Kristo, lakini walisahau kwa nini kazi hiyo ilikuwa muhimu.

- Yesu anazungumza kuhusu moja ya vitisho vikuu kwa utume wa kanisa: Mkristo mwenye kuridhika na nafsi yake (aliyejitosheleza).
    - Kutosheka kunamaanisha kupata kuridhika katika maisha tuliyo nayo badala ya maisha ambayo Yesu anatamani tuwe nayo.
    - Mkristo aliyejitosheleza si lazima awe mtu ambaye haendi kanisani kujihusisha na huduma.
    - Kumbuka, Efeso ilikuwa ikifanya matendo mengi, Yesu alisema
- Mkristo aliyejitosheleza amesahau kwamba Yesu ndiye msimamizi, wa kanisa na wa maisha yako
    - Unakuja kanisani kila juma, unaegesha gari lako sehemu ile ile, unasalimia watu wale wale, unakaa kwenye kiti kile kile.
    - Unaimba nyimbo zilezile, usema sala zile zile, unasikia mahubiri yaleyale ya motisha (kutia moyo) kila wiki, unatoa kiasi kile kile cha pesa.
    - Ni kustarehe (raha), haikuulizi chochote na iko chini ya udhibiti wako

- Na umeacha upendo wako wa kwanza…umesahau kwa nini unafanya jambo hili tunaloliita kanisa
    - Makanisa yanayoacha upendo wao wa kwanza ni makanisa yanayoanzisha zahanati au shule kama njia ya kuwafikia waliopotea
        - Lakini baada ya muda kazi inakuwa tu kuhusu kuponya majeraha ya kimwili au kufundisha ujuzi wa kidunia
        - Wanasahau kuhusu utume
    - Na kwa kiwango cha mtu binafsi, inaonekana kama programu za kanisa zinazosahau kushiriki Injili
        - Au madarasa ya Biblia au vikundi vidogo ambavyo havijawahi kusoma Biblia
        - Au vikundi vya wanaume na wanawake ambavyo vinajaza kalenda zao na viatu na viatu vya farasi na hawazungumzi kamwe juu ya Yesu.
        - Ni dhamira ya kumshirikisha Yesu na ulimwengu ndiyo sababu hata tunakusanyik…huo ndio upendo wetu wa kwanza.
    - Fikiria nyuma ambapo umeanguka…ni lini yote yalikuja tu kuhusu ushirika, utaratibu na mwonekano?
        - Na kama wewe ni kiongozi wa huduma au mwajiriwa wa kanisa, ni lini ilianza kuwa kazi na malipo?
        - Unaweza kuwa na shughuli nyingi zaidi kuliko hapo awali, lakini ni muda mrefu umepita tangu Yesu amekuwa akidhibiti kalenda yako au kuweka vipaumbele vyako.
        - Kutembea kwako kama Mkristo kumekuwa kwa mfumo wa kiotomatiki, na Yesu anasema anayo pingamizi juu yako kwa sababu hiyo.
    - Kumbuka Yeye huongoza Kanisa, na kwa kuwa wewe ni kiungo cha mwili, Yeye huendesha

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

maisha yako pia

- Lakini je, unamfuata Yeye? Je, unamsikiliza Roho?
- Tunapomfuata Yesu, Yeye hutuleta kutoka upeo wa macho hadi upeo wa macho, kutoka majaribu hadi majaribu, ushindi hadi ushindi.
- Kumfuata Yesu kamwe si jambo la kuchosha au jambo la kawaida, kwa sababu Yesu hatatuacha tupate kuridhika binafsi…Anataka tukue.

- Yesu anajali sana jambo hili, na analiambia kanisa lake kwamba kutakuwa na adhabu ikiwa watashindwa kutii wito wake wa kutubu.
  - Katika mst.5 Yesu anasema naja kwako ili kukiondoa kinara chako katika mahali pake usipotubu
    - Tunajua kinara cha taa ni ishara inayowakilisha kanisa lenyewe
    - Kwa hiyo, kuondoa kinara cha taa ni lazima kuwe na maana ya kumaliza mwili fulani wa kanisa
    - Na kwa kuwa kanisa hili lilikuwa kanisa la mji mzima, Yesu anatishia kuleta mwisho wa kanisa katika mji huo
  - Yesu alitaka Efeso itende kulingana na jina lao: walitamani
    - Yesu alitaka kanisa limtamani kama Paulo asemavyo:

> 1KOR. 2:1 **Basi, ndugu zangu, mimi nilipokuja kwenu, sikuja niwahubiri siri ya Mungu kwa ufasaha wa maneno, wala kwa hekima.**
> 1KOR. 2:2 **Maana naliazimu nisijue neno lo lote kwenu ila Yesu Kristo, naye amesulibiwa.**

- Kuna mambo mengi tunaweza kutamani katika maisha yetu ya kanisa, lakini hatuwezi kumwacha Yesu nyuma na kutarajia kuendelea kumtumikia.
- Basi nini kilitokea? Je, kanisa la Efeso lilitubu?
  - Hatuwezi kudhani tu, kwa sababu mwanzoni mwa karne ya pili, jiji lilikuwa katika hali ya kushuka kwa kasi
  - Mchanga ulianza kujaa katika bandari maarufu na yenye shughuli nyingi na kusababisha bandari yenyewe kurudi nyuma na kujitenga mbali na mji.
- Bandari iliposonga mbali zaidi na jiji, hatimaye ilipoteza chanzo chake kikuu cha mapato
  - Na kwa kifo cha biashara, mji hatimaye uliachwa
  - Magofu ya Efeso sasa yako maili nyingi sana ndani ya nchi badala ya pwani
  - Kama Yesu alivyoahidi, angekikomesha kile kinara, ambacho kinathibitisha kwamba anatembea kati ya makanisa yake akitawala.
- Hata hivyo, Yesu anatuambia kwamba haijalishi nini kinaweza kutokea kwa Kanisa mahali popote, uhusiano wetu wa kibinafsi na Yesu haubadiliki.
  - Katika mst.7 Yesu anawaita waamini wote (wale walio na masikio ya kusikia) akisema kwamba Roho anatuthibitishia kwamba tutakula matunda ya mti wa uzima.
    - Huu hapa ni muundo mwingine katika barua zote…zote huishia kwa kutia moyo waamini

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

wote kutazamia

- Haijalishi ni nini kingine kinachoweza kwenda mrama duniani katika makanisa yetu mbalimbali, mustakabali wetu wa milele uko salama
- Na katika wakati huo ujao wa milele, tutapokea yote ambayo yameahidiwa

- Katika kila barua saba, Yesu anarejelea mambo fulani kutoka kwenye makao ya milele ambayo tutajua wakati ujao
  - Hapa ni kumbukumbu ya mti wa uzima ambao sisi sote tutakula katika siku inayokuja
  - Badala ya kushughulikia maelezo hapa, nitahifadhi hiyo kwa ajili ya Sura ya 22

- Kwa hiyo tumeiangalia barua ya kwanza kwa mtazamo halisi, wa kihistoria na kwa mtazamo wa ulimwengu wote, usio na wakati, lakini vipi kuhusu mtazamo wa kinabii?
  - Je, kanisa hili linawakilisha vipi kipindi cha kwanza cha wakati wa kanisa?
    - Kwanza kabisa, ni rahisi kusema kanisa hili linawakilisha kipindi cha kwanza kati ya vipindi saba vya enzi ya kanisa kwa vile ni barua ya kwanza
    - Hiyo ingemaanisha kwamba hii ndiyo barua inayowakilisha asili ya kanisa tangu mwanzo wa kanisa hadi wakati fulani baadaye
  - Tunajua kanisa lilianza rasmi siku ya Pentekoste, kulingana na ufafanuzi wa Mkristo Paulo anaotupa katika Warumi

> RUM. 8:9 Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuati mwili; bali mwaifuata roho. Lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake.

> RUM. 8:14 Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu.

- Wale walio na Roho wa Mungu akiishi ndani yao ni Wakristo, na ni wana na binti za Mungu
- Na wote walio na Roho wa Mungu wanahesabiwa kuwa sehemu ya mwili mmoja uitwao kanisa

> EFE. 4:4 Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.
> EFE. 4:5 Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja.
> EFE. 4:6 Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote.

- Wale wote wenye Roho wa Mungu ni sehemu ya kanisa
  - Unapokuja kuamini kwamba Yesu ni Mungu na kwamba alikuja kuishi na kufa kama mwanadamu ili kukuokoa na dhambi zako
  - Kwa kifo chake alilipa gharama ambayo Mungu anadai kwa ajili ya dhambi yako na kwa ufufuo wake anathibitisha kwamba anaweza kukupa uzima wa milele

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

- Kwa imani yako katika Injili hiyo umezaliwa upya kiroho
- Na kama ishara ya awali ya mustakabali wa milele, Mungu hutuma Roho Wake kuishi ndani yako akikuunganisha na waamini wengine wote katika mwili mmoja.

- Kwa hiyo barua kwa Efeso inatupa muhtasari wa jumla wa jinsi kanisa kwa pamoja lilivyoibuka katika siku zake za kwanza.
  - Kanisa lilianza na upendo wake wa kwanza, likifahamu kikamilifu kwamba yote ni kuhusu Kristo na likingojea kwa hamu kurudi kwake
    - Kumbuka ufafanuzi huu kutoka kwenye kitabu cha Matendo ya Mitume:

---

MATENDO 2:41 Nao waliolipokea neno lake wakabatizwa; na siku ile wakaongezeka watu wapata elfu tatu.
MATENDO 2:42 Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.
MATENDO 2:43 Kila mtu akaingiwa na hofu; ajabu nyingi na ishara zikafanywa na mitume.
MATENDO 2:44 Na wote walioamini walikuwa mahali pamoja, na kuwa na vitu vyote shirika,
MATENDO 2:45 wakiuza mali zao, na vitu vyao walivyokuwa navyo, na kuwagawia watu wote kama kila mtu alivyokuwa na haja.
MATENDO 2:46 Na siku zote kwa moyo mmoja walidumu ndani ya hekalu, wakimega mkate nyumba kwa nyumba, na kushiriki chakula chao kwa furaha na kwa moyo mweupe,
MATENDO 2:47 wakimsifu Mungu, na kuwapendeza watu wote. Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa.

---

- Hivyo ndivyo inavyoonekana mtu anapoishi kwa ajili ya Kristo
- Na katika miaka ya kwanza ya kanisa, watu walikuwa wakiishi kana kwamba hakuna kesho duniani
- Kwa sababu walitarajia Yesu angerudi mara moja, na kurudi kwa Yesu kunapokuwa kwanza akilini mwako, basi hufikirii kidogo ulimwengu huu.
  - Walikuwa wakitumia muda wao daima katika kusali, na kudumu pamoja, wakishiriki yote waliyokuwa nayo, wakiuza mali zao.
  - Hiyo ni tabia ya mtu anayejua kuwa yote ni kuhusu Yesu
- Lakini baada ya muda, kanisa lilipoanza kutambua kwamba kurudi kwa Yesu kunaweza kuchukua muda mrefu kuliko walivyodhani, mambo yalibadilika
  - Na ilibidi…kanisa lilipaswa kuwepo ulimwenguni
  - Hii ina maana ilibidi kuweka usawa kati ya kutazamia umilele pamoja na Yesu na kuishi kwa leo
  - Hilo ndilo lilikuwa jambo la msingi la Kanisa kubaki nyuma wakati Yesu anaondoka…kwamba tungeshuhudia kwa ulimwengu

---

YOHANA 17:15 Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

uwalinde na yule mwovu.

YOHANA 17:16 Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu.

- Katika karne ya kwanza, kanisa la kwanza liliakisi mambo ambayo Yesu anawaambia Efeso katika barua hii
    - Kwa ujumla, kanisa lilishikilia mafundisho ya kweli, kwa kuwa Mitume wenyewe walikuwa hai, wakifundisha na kuliongoza kanisa
        - Walipinga mafundisho ya uongo huku wakihifadhi maandishi ya Mitume ili hatimaye kuunda maandiko matakatifu ya Agano Jipya.
        - Walifanya kazi za kuvutia katika kupeleka Injili nje kwa muda mfupi
        - Kanisa lilienea hadi Rumi na hata Uhispania kabla ya mwisho wa karne ya kwanza
    - Lilikuwa pia kanisa la ustahimilivu dhidi ya mateso ya Wayahudi na halikuchoka na mashambulizi yao
        - Mateso ya Wayahudi yalipotokea Yerusalemu, kanisa lilihamia Ughaibuni
        - Na baadaye wakati mateso ya Warumi yaliyoanzishwa na Nero yalipotokea, kanisa lilidumisha ushuhuda wake hadi kufa.
        - Ingawa walimu wa uongo walijaribu kujipenyeza ndani ya kanisa na kuanzisha uongozi usio wa kibiblia nyakati fulani, kanisa lilibaki imara.
        - Kwa hiyo mambo chanya ambayo Yesu alisema juu ya Efeso kwa ujumla yalikuwa yanawakilisha asili ya kanisa la kwanza kwa ujumla
    - Lakini karne ilipoendelea na mtume wa mwisho kufa, kanisa lilianza kubadilika kwa njia ambazo pia zinaakisi maoni hasi ya Yesu
        - Wakristo wa Kiyahudi kwa kiasi kikubwa walikufa, huku wapagani, Warumi walianza kuongoka na kuingia kanisani kwa maelfu
        - Waumini hawa wa Mataifa walikuwa tayari zaidi kuliko watangulizi wao wa Kiyahudi kuchanganya Ukristo na utamaduni wa Kirumi
    - Kama matokeo ya kufanya hivyo, kanisa likawa sehemu ya jamii ya Warumi
        - Katika miji kama Efeso, kanisa lilipata nafasi kando ya mahekalu ya Warumi na serikali
        - Na waumini walibakia kuwa wachanga na wa kimwili
        - Tunaweza kuona jambo hili waziwazi katika barua ambazo Paulo aliandikia moja ya makanisa ya Wamataifa na Warumi ya siku hizo, Korintho.
        - Waumini walikuwa wameridhika, wakiwa na shughuli nyingi katika ujenzi wa kanisa, lakini kwa njia hiyo hiyo Warumi walijenga jamii ya Warumi…
        - … kwa ajili yake tu
- Kwa hiyo Yesu alifanya nini ili kutikisa mambo katika kanisa lake? Huko Efeso, Bwana aliondoa mahali pa kanisa
    - Na kwa kanisa kwa ujumla, Bwana aliondoa nafasi ya kanisa ya upendeleo na usalama katika Milki ya Roma.
        - Bwana aliruhusu mateso ya kudumu, yaliyoenea sana kuingia kanisani na kulivunja kanisa

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

huru kutokana na kujitosheleza kwake.

- Kanisa halikuwa tena limejiridhisha na limejistarehesha wala halikuweza kupata nafasi katika jamii ya Warumi
- Badala yake lilienda kwa siri na wale ambao hawakuwa wa Kristo kweli kweli kwa haraka walikata tamaa.

- Kilichobaki kilikuwa ni mwili wa kweli, uliojitolea ambao ghafla unakumbuka maana ya kuwa mtumwa wa Kristo
  - Na ilimaanisha nini kuteseka kwa ajili ya Kristo
  - Na hiyo inatupeleka kwenye kanisa la pili, lile linaloitwa Smirna, ambalo maana yake ni "kifo".
- Basi, ni kipindi gani cha historia tunachoiweka barua hii ya kwanza ya kanisa?
  - Tarehe ya kuanza ni rahisi, kwa kuwa ni kipindi cha kwanza cha kanisa na kanisa lilianza Pentekoste
  - Nitatumia makadrio ya takwimu za jumla kwani tarehe kamili haijulikani na sio muhimu
  - Kwa hiyo tunaweza kusema Kanisa lilianza karibu 30 AD
- Lakini linamalizika (linaisha) lini? Hakuna sayansi kamili ya kuchagua tarehe hizi
  - Lengo ni kuunganisha tarehe zetu na tukio fulani la kihistoria linalofungamana na maelezo ya barua.
  - Ni tukio gani linaweza kuashiria mwisho wa kipindi cha kwanza cha kanisa?
- Tunajua kwamba mabadiliko muhimu kati ya kipindi cha kwanza na cha pili ni kuongezeka kwa mateso
  - Na tunapojifunza Smirna wiki ijayo, tutaona mabadiliko hayo waziwazi
  - Lakini hakuna siku moja maalum ambayo mateso yalianza, kwa hiyo hatuna alama bayana ya tarehe hiyo.

- Lakini kuna alama moja ambayo inaashiria wazi hatua ya mabadiliko kwa kanisa la awali: mwisho wa mitume
  - Yohana alipokufa, mtume wa mwisho alikuwa ameondoka na kwa mara ya kwanza kanisa lilikuwa bila uongozi wa kitume
    - Mahali pao (yaani mitume) tulikuwa na kitu muhimu zaidi na chenye nguvu zaidi cha kuliongoza kanisa: neno la Mungu
    - Mitume walikuwa manabii wa Agano Jipya ambao waliotoa kanoni ya Agano Jipya
    - Na mara tu mtume wa mwisho, Yohana, alipoandika kitabu cha mwisho cha Maandiko (Ufunuo) hitaji la mitume liliisha
  - Isitoshe, kifo cha Yohana mwishoni mwa karne ya kwanza pia kiliambatana na utawala wa kigaidi ulioletwa na Kaisari Domitian.
    - Utawala huo ulianzisha kipindi kibaya cha mateso ya Warumi ambayo yalizidi na baadaye kupungua kwa karne mbili zilizofuata.
    - Kwa hiyo kwa kuzingatia maelezo hayo, tunaweza kuweka tarehe ya kipindi cha kwanza cha historia ya Kanisa iliyotabiriwa na barua ya Yesu kwa Efeso  kuwa kati ya mwaka 30-100 BK.

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org

    - Na tunaweza kukiita kipindi hiki "Enzi ya Kitume".
- Kwa hiyo wakati unaoliunganisha kanisa kutoka kwa Ujio wa Kwanza wa Kristo hadi Ujio Wake wa Pili unaanza na kipindi cha Efeso.
    - Na wiki ijayo tunahamia kipindi cha pili, cha tatu na cha nne

© 2019 – Verse By Verse Ministry International (www.versebyverseministry.org)
May be copied and distributed provided the document is reproduced in its entirety, including this copyright statement, and no fee is collected for its distribution.
Scripture quotations taken from the (NASB®) New American Standard Bible®, Copyright © 1995, 2020 by The Lockman Foundation.
Used by permission. All rights reserved. www.lockman.org